TANGAZO LA SERIKALI NA. ....109........la tarehe....18/07/08........

HALMASHAURI YA WILAYA KIBONDO 21/7/08

GOVERNMENT PRINTER
CHAPISHA KATIKA GAZETI LA
Tarehe 18/7/2008
Mhariri

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
( SURA YA 290)

Zimetungwa chini ya vifungu vya 6(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA KIBONDO, 2008

Jina

**1.** Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo (Ushuru wa mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2008.

Matumizi

**2.** Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

**3.** Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo-

"daftari au leja" maana yake ni daftari au leja iliyoanzishwa na Halmashauri au Halmashauri ya Kijiji au Afisa Mtendaji wa Kata kwa ajili ya kusajili wanunuzi wa mazao katika eneo la Halmashauri;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya Kibondo;

"Mkurugenzi" maana yeke ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo au mtu yeyote anayekaimu nafasi hiyo;

"Mamlaka husika" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji, Kamati ya Maendeleo ya Kata, Afisa Mtendaji wa Kijiji, Afisa Mwidhiniwa au Mamlaka yo yote;

"Afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa Kilimo wa Wilaya, Mweka Hazina wa Halmashauri pamoja na Afisa Biashara wa Wilaya na Afisa Mtendaji wa Kata,au Afisa yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kushughulikia ushuru wa mazao;

"mkusanya ushuru" maana yake ni mkusanya ushuru wa mazao aliyeteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru wa mazao katika Halmashauri;

"mnunuzi" maana yake ni mtu yeyote au taasisi yoyote inayonunua mazao ya Kilimo ambalo yaliyoorodheshwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi katika eneo la Halmashauri;

"muuzaji" maana yake ni mtu yeyote anayeuza mazao ya Kilimo katika eneo la Halmashauri;

"zao" maana yake ni zao lolote la Kilimo ambalo limeainishwa kwenye Jedwali la Kwanza na la Pili la Sheria Ndogo hizi.

**4.** –(1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kutakuwa na ushuru utakaotozwa na kukusanywa kutoka kwa kila mnunuzi wa zao lolote lililoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi kwa kiwango cha asilimia tano kwa mia moja (5%) ya bei ya kununulia shambani (farm gate price).

(2) Bila ya kuathiri kifungu cha 4(1) cha sheria ndogo hizi ushuru wa mazao yote yaliyoorodheshwa katika Jedwali la Pili utakuwa ni kwa kiwango cha asilimia tano kwa mia moja(5%) kwa kila gunia.

(3) Ushuru wa zao la pamba, kahawa na tumbaku utalipwa kwa Halmashauri ndani ya muda wa kipindi cha siku sitini (60) baada ya kahawa au tumbaku kuuzwa na muuzaji mnadani au kwa mnunuzi ye yote na endapo muda huo utapita bila ushuru kulipwa mnunuzi atatozwa na Halmashauri riba ya 10% ya ushuru huo endapo atakuwa amedaiwa ushuru huo kwa maandishi na bila sababu yo yote mnunuzi hakuweza kulipa ushuru huo ndani ya muda wa notisi ya kumtaka alipe ushuru.

(4) Ushuru utakaotozwa kwa ajili ya zao lingine lolote mbali na pamba, Kahawa au tumbaku utalipwa kabla ya zao hilo halijasafirishwa kwenda nje ya eneo la Halmashauri au kabla ya zao hilo kuwekwa katika ghala kwa ajili ya kusafirishwa baadaye.

Wajibu wa mnunuzi kujisajili

**5.**–(1) Bila ya kujali eneo la makazi ya mnunuzi litakuwa ni Sharti la Kisheria chini ya Sheria Ndogo hizi kila mnunuzi kujisajili katika daftari au leja ya Halmashauri ya Wilaya au Halmashauri ya Kijiji kwa ajili ya kununua zao lolote lililotajwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi na baada ya kusajiliwa atapewa kibali cha maandishi au kibali maalum kilichotengenezwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Baada ya Mnunuzi kupata kibali au usajili, ataorodheshwa na Afisa Mtendaji wa Kata au Kijiji katika daftari la Kata au Kijiji kama mnunuzi wa mazao ambayo itaonyesha taarifa zifuatazo-

(a) Jina;
(b) sahihi na anuani ya mnunuzi;
(c) kiwango cha mazao anayotegemea mnunuzi kununua na tarehe anayotarajia kusafirisha;
(d) namba ya kibali; na
(e) Orodha na namba za magari atakayotumia kusafirisha mazao hayo.

**6.**-(1) Ushuru utakaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Mkurugenzi Mtendaji au kwa mkusanya ushuru.

(2) Kila mnunuzi atakayelipa ushuru wa mazao chini ya Sheria Ndogo hizi atapewa stakabadhi ya ushuru kwa ajili ya mazao aliyonunua.

(3) Haitakuwa utetezi au kinga kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kwa mnunuzi kudai kwamba amenunua mazao lakini hakupewa stakabadhi au kwamba amepewa stakabadhi isiyolingana au kuwiana na kiwango cha mazao aliyonunua.

(4) Endapo afisa muidhiniwa au mkusanya ushuru atabaini kuwa mnunuzi hajalipa ushuru au amelipa ushuru wa mazao usiolingana na kiwango cha mazao aliyonunua-

(a) atamtaka mnunuzi huyo kulipia ushuru wa mazao mara moja na kumkatia stakabadhi; na

(b) anaweza kukamata mazao hayo na kuyahifadhi chini ya mamlaka ya halmashauri kwa muda usiopungua siku 14 (kumi na nne).

(5) Endapo mazao yaliyokamatwa kwa sababu ya kutolipiwa ushuru wa mazao hayatalipiwa ushuru huo ndani ya muda wa siku 14 tangu yalipokamatwa-

(a) yatauzwa na Halmashauri kwa njia ya mnada na ushuru huo kukatiwa stakabadhi kama mapato ya Halmashauri; na

(b) mnunuzi wa mazao atachukuliwa hatua za kisheria kwa kukwepa kulipa ushuru.

Wajibu wa Mkusanya Ushuru

7.-(1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa-

(a) kuteua mtu yeyote kuwa mkusanya ushuru wa mazao katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri;

(b) kuteua taasisi au Chama chochote cha Ushirika au SACCOs kuwa mkusanya ushuru wa mazao;

(c) kumchukulia hatua za kisheria mkusanya ushuru wa mazao au mtu ye yote ambaye atakiuka Sheria ndogo hizi; na

(d) kufuta au kusitisha mkataba wa kukusanya ushuru kwa mkusanya ushuru yeyote wakati wo wote ule itakapothibitika kuwa ameshindwa kukusanya ushuru kwa sababu yoyote ile.

(2) Kila mkusanya ushuru atakuwa na wajibu wa-

(a) kutoa taarifa ya maandishi kwa Halmashauri juu ya orodha ya majina ya wanunuzi wa mazao waliopo katika eneo ambalo ameteuliwa kukusanya ushuru wa mazao ambao wanapaswa kulipa ushuru;

(b) kukusanya na kupokea ushuru wa mazao kutoka kwa kila mtu anayetakiwa kulipa ushuru kwenye eneo aliloteuliwa kukusanya ushuru wa mazao;

(c) kuwasilisha taarifa katika Halmashauri kuhusu jina la mtu yeyote atakayeshindwa au kukataa kulipa kiasi chochote cha ushuru unaodaiwa;

(d) kutoa ushuru kwa mnunuzi wa mazao yaliyoidhinishwa au kuorodheshwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi; na

(e) kuwasilisha Ushuru uliokusanywa kwa Halmashauri kwa mujibu wa mkataba.

(3) Bila kuathiri masharti ya fungu la 7 (1) na (2) ya Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itakuwa na Mamlaka na wajibu wa kuhakikisha kwamba, malipo na vigezo vingine vyovyote vinavyohusiana na taratibu za ukusanyaji wa ushuru vitaonyeshwa kwenye mkataba wa ukusanyaji ushuru utakaofanywa kati ya Halmashauri na mkusanya ushuru husika.

Mamlaka ya Mkurugenzi

**8**. Mkurugenzi atakuwa na haki, Mamlaka, wajibu na uwezo wa-

(a) kuomba au kumtaka mtu yeyote atoe taarifa inayohusu ununuzi wa malipo ya ushuru wa mazao wakati wowote;
(b) kumtaka mtu yeyote ambaye ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kulipa kiasi cha fedha ambacho hakizidi kiwango cha juu cha faini kilichotajwa kwa ajili ya kosa hilo pamoja na ushuru anaodaiwa;
(c) kuamuru kukamatwa kwa mazao yaliyonunuliwa lakini hayajalipiwa ushuru wa mazao;
(d) kumtaka mtu yeyote kukiri kosa kwa kutumia fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la sheria ndogo hizi; na
(e) kuchukua hatua ya kisheria dhidi ya mtu yeyote katika mahakama kuhusu ukiukaji wowote wa Sheria Ndogo hizi.

**9**.-(1) Kila mnunuzi atakuwa na wajibu wa kutunza au kuhifadhi stakabadhi na kibali cha kununua mazao kilichotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa ajili ya ukaguzi mahali popote na wakati wowote.

(2) Hakuna ushuru utakaohesabika kwamba umelipwa kama stakabadhi kwa ajili ya malipo hayo haitawasilishwa kwa Afisa Mwidhiniwa au Mkurugenzi kwa ajili ya Ukaguzi.

Makosa na adhabu

**10**.–(1) Mnunuzi yeyote atakayeshindwa au atakayekataa kulipa ushuru wa mazao ambao unapaswa kulipwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa akitiwa hatiani atatakiwa kulipa faini kwa kiwango kisichozidi shilingi laki tatu 300,000/= au kutumikia kifungo cha muda usiozidi miezi kumi na mbili jela au faini na kifungo kwa pamoja.

(2) Mkusanya ushuru yeyote aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi-

(a) atakayeshindwa kuwasilisha kwenye Halmashauri kiasi chochote cha ushuru uliokusanywa au uliotakiwa kukusanywa; au
(b) ambaye atazembea au atatoa taarifa za uongo kwa makusudi kuhusu idadi ya walipa ushuru au kiasi cha ushuru alichokusanya; au
(c) ambaye kwa makusudi atashindwa kutekeleza kazi zozote alizopewa kama mkusanya ushuru,

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini ya kiwango kisichopungua au kuzidi shilingi laki tatu au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili jela au faini na kifungo vyote kwa pamoja.

(3) Bila ya kuathiri masharti yoyote ya Sheria Ndogo hizi Afisa Mwidhiniwa au mtumishi yeyote wa Halmashauri atakayeidhinishwa au kuteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza Sheria Ndogo hizi anaweza wakati wowote kwenda kwenye eneo lolote la halmashauri kwa lengo la kufanya ukaguzi, kupata takwimu au taarifa sahihi juu ya mwenendo mzima wa ukusanyaji wa ushuru.

**11.** Mtu yeyote yule ambaye ni mkusanya ushuru au mnunuzi wa mazao ambaye-

(a) atashindwa au kukataa kulipa ushuru kwa makusudi;
(b) atashawishi kundi la watu au mtu kutotoa taarifa au kusafirisha mazao ambayo hayakulipiwa ushuru;
(c) atashawishi mtu au kundi la watu kutoa taarifa ya uongo kuhusu ushuru au kiasi cha mazao yaliyonunuliwa;
(d) atamzuia Afisa Muidhiniwa au mkusanya ushuru asitekeleze jukumu lake chini ya sheria ndogo hizi;
(e) atakiuka sheria ndogo hizi; au
(f) atasafirisha mazao usiku,

atakuwa ametenda kosa na atashitakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atalazimika kulipa ushuru anaodaiwa pamoja na faini isiyozidi shilingi 300,000/=, au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au kifungo na faini vyote kwa pamoja.

**12.** Sheria Ndogo hizi hazitaathiri au kutafsiriwa kwa maana ambayo inaathiri haki ya Halmashauri ya kudai, ushuru au nafuu nyinginezo kwa kufungua shauri la madai chini ya masharti ya Sheria ya Kanuni ya Mwenendo wa Sheria ya Madai (Civil Procedure Code, 1966, cap 33 R.E 2002); Amri ya XXXV kama Halmashauri itakavyoona inafaa.

Tangazo la Serikali No. 284 la mwaka 1994

**13.** Sheria Ndogo (Ushuru wa Mazao ya Kilimo) za Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo za mwaka 1994 na marekebisho yake yote zinafutwa.

**JEDWALI LA KWANZA**

*(Chini ya kifungu cha 4(1))*

Mazao yanayotozwa ushuru wa asilimia tano ya bei ya kununulia (farmgate price)

(1) Kahawa
(2) Tumbaku
(3) Pamba

**JEDWALI LA PILI**

*(Chini ya kifungu cha 4(2))*

(1) Mahindi
(2) Maharage
(3) Mpunga/Mchele
(4) Makopa ya muhogo
(5) Ulezi
(6) Karanga

(7) Mtama wa aina yoyote
(8) Njegele
(9) Kunde na mbaazi
(10) Na vinginevyo vinavyouzwa sokoni kwa ujazo wa gunia

**JEDWALI LA TATU**

KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO

*(Chini ya fungu la 5 (1))*

HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO

S.L.P. 43,
**KIBONDO.**

Kibali Na. ......................................
Tarehe..........................................

**YAH: KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO**

**HII NI KUTHIBITISHA** Kwamba leo hii tarehe ...........Mwezi............. mwaka.............. Ndugu......................................................wa S.L.P............ ambaye amejitambulisha kwa Mkurugenzi na kuomba kupewa kibali cha kununua mazao aina ya ......................................... katika Kata/Soko....................................... amepewa kibali hiki na Afisa Mwidhiniwa au Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya na Kibali hicho hakitatumika katika eneo lolote ambalo mnunuzi hakuomba kwa ajili ya kununua mazao ndani ya eneo lililo katika Mamlaka ya Halmashauri na kitaishia tarehe........................ Mwezi....................mwaka..................

- Gari/magari atakayotumia, .....................(idadi)
- Namba za Usajili.........................................

.............................................
**MKURUGENZI MTENDAJI/AFISA MWIDHINISHA**

Tarehe...............................
Muhuri .............................

**JEDWALI NNE**

(Chini ya Kifungu cha 9 (e)

**HATI YA KUKIRI KOSA**

Mimi ..................................................... wa S.L.P. ................................ nakiri mbele ya Ms.................................................. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kibondo kwamba mnamo tarehe .................... mwezi ............... Mwaka......... Nilitenda kosa kwa kukiuka kifungu cha ..............................cha Sheria Ndogo (Ushuru wa mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo za mwaka 2007.

Kutokana na ukiukaji huo nipo tayari kulipa kiasi ninachodaiwa ikiwa Mkurugenzi Mtendaji ataamua kutekeleza madaraka yake aliyopewa chini ya Kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo zilizotajwa hapo juu na Kifungu cha 153 (2) cha Sheria Na. 7 ya 1982.

Nathibitisha kwamba yote niliyosema ni kweli kadri ya ufahamu wangu na nimeyasema bila kulazimishwa na yeyote kwa namna yoyote ile.

Nembo ya Halmashauri imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika tarehe ........21.........mwezi .........4..........mwaka 2007 na imebandikwa mbele ya

PAUL NKULILA
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**KIBONDO**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KIBONDO

SAIMON KANGUYE KAGOLI
**MWENYEKITI WA HALMASHAURI**
**YA WILAYA KIBONDO**

MWENYEKITI WA HALMASHAURI
YA WILAYA KIBONDO

***NAKUBALI:***

**MIZENGO KAYANZA PETER PINDA (MB)**
**WAZIRI MKUU**

**DODOMA**

…...………..2008